TANGAZO LA SERIKALI NA. 212 la tarehe 22/3/2024

SHERIA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1)*

SHERIA NDOGO YA USAFI NA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA UJIJI YA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujiji ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama utahitaji vinginevyo:

"ada ya kuondoa taka" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka.

"ada ya uchafuzi wa mazingira" maana yake ni malipo yanayotakiwa kulipwa kwa Halmashauri na kampuni, viwanda, kikundi, mtu binafsi au taasisi ambazo shughuli zao zinasababisha uchafuzi wa mazingira; .

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"ardhi tengwa" maana yake ni sehemu ya ardhi ambayo imetengwa maalum kwa ajili ya hifadhi ya mazingira;

Sura 191

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"bioanuwai" maana yake ni tofauti kati ya viumbe hai kutoka vyanzo vyote ikiwa ni pamoja na mifumoikolojia ya nchi kavu, mifumoikolojia ya majini na ikolojia changamani ambayo ni sehemu ya mifumoikolojia hiyo;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii ikiwemo visima, mito, chemchemi, vijito na maeneo yote yanayopatikana maji;

"chombo cha taka ngumu" maana yake ni chombo maalum kwaajili ya kuhifadhia taka ngumu kwenye kaya, shughuli za kiuchumi na maeneo ya wazi;

"choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu;

"dampo"maana yake ni eneo la kuteketezea taka;

"elimu ya mazingira" maana yake ni elimu itakayohusu mchakato wa kutambua sifa na kufafanua dhana ya mazingira ili kuboresha taaluma na mtizamo muhimu kwa ajili ya kuelewa na kukubali uhusiano kati ya binadamu, utamaduni na hali hai inayomzunguka;

"eneo la hifadhi'' maana yake ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya

misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujiji;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi; mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria ya Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"huduma" maana yake ni kuondoa na kuteketeza taka za viwandani, biashara, majumbani na sehemu nyinginezo ambazo zinazalisha taka;

"jengo la biashara" maana yake jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya biashara iliyokusudiwa;

"kaya" maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye eneo la Halmashauri;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha:

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;

(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa;

(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"kikundi cha mazingira" maana yake ni kikundi

chochote cha watu kilichosajiliwa kufanya usafi na usimamizi wa mazingira na udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;

"kizimba cha taka" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu;

"kituo cha maji machafu" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengenezwa kwa ajili ya ukaguzi wa mfereji ambao una mfuniko usioruhusu hewa kutoka;

"kuchakata taka" maana yake ni kuzichambua, kuzitenganisha na kuzibadili kuwa kitu kingine chenye manufaa kwa jamii;

"mabwawa ya maji taka" maana yake ni mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani na viwanda;

"maeneo ya shughuli za kiuchumi" ni maeneo maalumu yaliyotengwa na Manispaa kwaajili ya shughuli za uzalishaji mali na kuingiza kipato.

"maeneo ya wazi" ni maeneo yanayomilikiwa na Manispaa ya Kigoma Ujiji na hayajaendelezwa.

"maeneo nyeti" maana yake ni maeneo oevu, mitelemko ya milima, misitu au maeneo maalumu yaliyotengwa kwa minajili ya misitu au bustani.

"mfumoikolojia" maana yake ni elimumwendo changamani ya jamii za mimea, wanyama, vijiumbe na mazingira yao vikiwemo vitu visivyo hai;

Sura 191 "maji" ina maana swa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 "maji taka" ina maana swa kama ilivyotafsiriwa katika

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mazalia ya wadudu" maana yake ni sehemu ambayo wadudu hufanya mazalio au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae huleta maadhara kwa binadamu;

Sura 323

"mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu na ni pamoja na kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa pamoja na miti, mazao yanayoota kupatikana msituni, ambao ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la misitu;

Sura ya 191

"mazingira" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anaejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, punda, nguruwe, mbuzi, mbwa, kondoo au kuku na wanyama wengine wote wafugwao majumbani;

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 na miti, uoto wa asili au uliopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota au ambayo itajumuisha na yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangaza chini ya sheria za misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au

anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujiji au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"mzalishaji wa taka ngumu" maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara au kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake za kila siku huzalisha taka ngumu;

"mtandao wa maji taka" maana yake mfumo wa bomba kuu lililojengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha taka miminika toka kwenye mifereji ya maji na kuyapeleka kwenye mabwawa ya maji taka au baharini;

"mzalishaji wa maji taka" maana yake mtu, shirika, kiwanda au taasisi ambapo shughuli zake kwa namna yoyote ile huzalisha maji taka;

"pipa la taka" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

"sehemu ya kufulia" maana yake ni eneo au jengo au chumba maalum kilichotengwa kwa ajili ya kuoshea au kufulia nguo;

Sura ya 191 "taka" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"taka za biashara" maana yake ni aina yoyote ya taka ambazo hupatikana au hutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara;

"Taka gesi" maana yake ni hewa chafu, moshi, joto, au harufu ambayo inaweza kuleta madhara kwa Binadamu, mazingira, na viumbe hai wengine;

"taka miminika" maana yake maji yaliyokwisha tumika au chafuliwa kwa namna yoyote ile ambayo

yanajumuisha maji machafu toka chooni, bafuni, jikoni, viwandani, maji yaliyooshewayo vyombo, maji yaliyofuliwa nguo, kuosha nywele, kuoshea vyakula na yaliyopigiwa deki na kutoka kwenye taasisi mbalimbali;

Sura ya 191 "taka ngumu" ina maana sawa kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"taka za majumbani" maana yake mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, nguo chakavu, karatasi za aina mbalimbali, kinyesi cha mifugo, taka za bustani na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

Sura ya 191 "taka za viwandani" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191 "uchafu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira ;

"uchafuzi wa mazingira" maana yake hali ya kusababisha mabadiliko hasi ya hali ya hewa, na uoto wa asili, au uwepo wa kelele au kero za aina yeyote, harufu mbaya, uwepo wa taka za aina yoyote, ambapo unasababisha hali ya hatari kwa afya binadamu na viumbe hai wengine;

"ukaguzi wa mazingira" maana yake ni tathmini yenye lengo, utaratibu, kumbukumbu, inayofanyika vipindi maalumu kwa madhumini ya kufahamu ni kwa kiasi gani mpangilio wa kimazingira, usimamizi na maandalizi yanavyofanywa katika kuhifadhi na kulinda mazingira;

"ufugaji endelevu" maana yake ufugaji unaofuata taratibu kwa mujibu wa sheria ya mifugo;

"ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya nyumba, banda au zizi ndani ya eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

Sura ya 191 "vitu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika

Sheria ya Mazingira ;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

## SEHEMU YA PILI
## UFUGAJI

Wajibu wa Halmashauri

4.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za malisho ndani ya eneo la Halmashauri;
(b) kutenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani;
(c) kufanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii;
(d) kujenga majosho ya mifugo kwa kushirikiana na wananchi;
(e) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii ili kuongeza tija;
(f) kutoa chanjo kwa kushirikiana na wafugaji ili kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyoambukiza na yanayoambukiza binadamu; na
(g) kudhibiti uzururaji holela wa mifugo na wanyama katika Halmashauri kwa mujibu wa Sheria.

Wajibu wa mfugaji

5. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hii atatakiwa-

(a) kufuga na kulisha mifugo katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;
(b) kupitisha mfugo au mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(c) kuwa na kadi ya mfugo au mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(d) kupeleka mfugo au mifugo katika josho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;
(e) kuchangia gharama za ukarabati wa josho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;
(f) kupeleka mfugo au mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;
(g) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
(h) kuweka alama kwenye mfugo au mifugo yake na katika viungo vya mfugo au mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;
(i) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyohitajiwa na Halmashauri;
(j) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o; na
(k) kusajili mfugo au mifugo katika rejista ya Kijiji, kuogesha mfugo au mifugo katika majosho kama ratiba itakavyopangwa.

Taratibu za Ufugaji

6.-(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hii.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na mtu yeyote hataruhusiwa kuchinja mfugo au mifugo mahali pengine popote ambapo sio machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa

Mwidhiniwa na atalazimika kulipia gharama za machinjio kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria ndogo hii.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kununua, kuuza au kufanya Biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

(4) Mfugaji atawajibika kumfungia mbwa wake kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa nne kamili usiku na atamfungulia kuanzia saa nne kamili usiku na kumfungia saa kumi na mbili kamili asubuhi.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

7.-(1)Halmashauri itakamata mfugo au mifugo yoyote itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa mahali pasipostahili utalipiwa faini ya Shilingi elfu ishirini kwa kila mfugo baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mfugo wake.

(3) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(4) Bila kuathiri aya ndogo ya (2), Halmashauri kabla ya kuuza mfugo huo kwa mnada itamjulisha mmliki na umma juu ya kusudio hilo.

(5) Endapo mifugo au mfugo atakufa, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama kifo hicho kitakuwa kimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

## SEHEMU YA TATU
## KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

Taratibu za Kilimo

8. Mtu yeyote atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia sheria husika.

Marufuku

9.-(1) Mtu yeyote hatoruhusiwa kulima katika miteremko, au karibu na vyanzo vya maji au kandokando ya mito au mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia ardhi kinyume na matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa nne kamili asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

(7) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa mabaki ya vifungashio vya viuatilifu au kusafisha vipulizi au kumwaga mabaki ya viuatilifu katika chanzo cha maji au mto.

## SEHEMU YA NNE
## HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

10.-(1) Halmashauri itawajibika, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

(3) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri na jamii husika kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(4)Mtu yeyote hataruhusiwa kumiliki eneo la chanzo cha maji.

Kulinda eneo la hifadhi

11. Mtu yeyote hataruhusiwa kulima au kukata miti au kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka chanzo cha maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

12.-(1) Mtu yeyote hatoruhusiwa-

(a) kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(b) kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai

## SEHEMU YA TANO
## HIFADHI YA MISITU

Kuchoma au Kusababisha moto

13.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchoma au kusababisha moto katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwananchi kuzima moto ambao utaonekana kuwaka katika eneo la Halmashauri yenye kuleta viashiria vya hatari.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika zoezi la kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Uvunaji miti

14.-(1)Mtu yeyote hataruhusiwa-

(a) kukata miti katika eneo la Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali; au

(b) kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali ya Taifa.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Mtu yoyote anaetaka kuvuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, mbao au kuni atatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo na atatakiwa kulipa ada ijulikanayo kama ada ya uvunaji miti kwa kiwango kilichoainishwa kwenye Jedwali.

Wajibu wa kupanda miti

15. Itakuwa ni wajibu wa:

(a) kila mkazi ndani ya eneo la Halmashauri, kupanda na kutunza miti katika eneo lake, makazi yake, shamba au mashamba anayoyamiliki;

(b) kila mmiliki wa jengo la makazi au biashara, kutunza na kupanda miti katika eneo lake.

Tathimini ya athari kwa mazingira na jamii

16.-(1) Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri haitaaendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira.

(2) Kila mpendekezaji wa mradi atawajibika kulipa Halmashauri asilimia kumi ya gharama ya tathimini ya athari za mazingira kama ada ya ukaguzi na usimamizi wa mradi husika.

Uhifadhi wa mazingira ya mto/bwawa na udhibiti wa rasilimali zake

17. Mtu yeyote hataruhusiwa-

(a) kutumia uvuvi wa juva, baruti, sumu au mkuki;
(b) kuvulia nyavu kwenye maji mafupi au kwenye miamba;
(c) kuvua, kuokota, kuchukua au kufanya kitendo chochote kwenye maeneo tengefu ya samaki isipokuwa kwa kibali maalum cha Halmashauri;
(d) kuvua samaki bila kuwa na leseni ya uvuvi; na
(e) kutumia chombo cha uvuvi kisichokuwa na namba za usajili pamoja na leseni ya chombo hicho.

Usafi na hifadhi ya Ziwa Tanganyika

18.-(1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kutunza na kusafisha fukwe na mialo katika maeneo ya pwani ya Ziwa Tanganyika.

(2) Mtu yoyote hataruhusiwa-

(a) kufanya shughuli za biashara katika maeneo ya fukwe na mialo bila kibali cha Halmashauri;
(b) kutiririsha maji machafu au Kemikali au mafuta au kutupa taka ya aina yoyote katika maeneo fukwe au ndani ya Ziwa Tanganyika;
(c) kuosha magari au pikipiki au mitambo ya aina yoyote katika fukwe za Ziwa

Tanganyika ;

(d) kulima, kuosha vyombo vya majumbani, kufua, au kufanya shughuli zote za kibinadamu isipokuwa zinazohusiana na uvuvi ndani ya mita 60 kutoka kingo za Ziwa Tanganyika.

(e) kuvua samaki, kwa kutumia mabomu, kemikali au mbinu zisizoruhusiwa kisheria;

(f) kuchimba mchanga au udongo kwenye maeneo ya fukwe au maeneo yaliyomo ndani ya mita sitini kutoka katika kingo ya ziwa; au

(g) kufanya shughuli yoyote itakayoathiri au inayoweza kuathiri mazingira na usalama wa Ziwa Tanganyika, samaki na viumbe wengine hai.

## SEHEMU YA SITA
## USIMAMIZI WA TAKA NA USAFI WA MAZINGIRA

Usafi wa mazingira

19. Kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki jengo au eneo la biashara atahahakisha kwamba-

(a) majani yanayozunguka jengo lake au makazi yanakatwa au kupaliliwa na kuondolewa katika eneo lake lote;

(b) taka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka;

(d) anaboresha na kupaka rangi jengo lake kila inapochakaa;

(e) ana choo kilicho bora na kisafi wakati wote;

(f) anashiriki siku ya usafi ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi;

(g) anaondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika mfereji wa maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa safi wakati wote;

(h) hakuna mkusanyiko wa maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla;

(i) anafanya uchambuzi wa taka;

(j) ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lilotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka;

(k) anatunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri; na

(l) kwa mfanyabiashara wa wa matunda au miwa, ana chombo maalumu cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Ada ya uzoaji taka

20.-(1) Kutakuwa na ada ya uzoaji taka ambayo itatozwa na Halmashauri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

(2) Ada ya uzoaji taka italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki na atajaza katika rejista ya

wazalishaji taka.

(3) Endapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Kutiririsha maji taka

21.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kutiririsha au kumwaga au kuruhusu au kusababisha kutiririsha au kumwaga maji taka barabarani, uchochoroni kwenye mifereji, mtoni, kwenye vyanzo vya maji au sehemu yoyote isiyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(2) Kila kiwanda kinachozalisha maji taka kitakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kinaunganisha maji taka au kujenga mifereji na mabwabwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka.

(3) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo la kuhifadhi linapojaa na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha karo kujaa na kutiririsha maji taka barabarani au sehemu yoyote isiyoruhusiwa.

Taka za viwanda

22.-(1) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na taka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

(2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha marufuku kuwa kiwanda chochote hakitoi au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya, vumbi au kelele na kusababisha kero kwa wakazi.

Taka hatarishi

23. Mtu yeyote, wakala au taasisi haitaruhusiwa kuendesha shughuli za uchomaji wa taka hatarishi bila

ya kupata kibali kutoka Halmashauri.

Ukusanyaji na uzoaji wa taka katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi

24.-(1) Halmashauri itasimamia shughuli za ukusanyaji na uzoaji wa taka kutoka katika maeneo ya masoko, asasi, maeneo ya biashara, na maeneo mengine yenye watu wengi ambapo taka zitakusanywa sehemu maalum na kuzolewa kulingana na aina ya taka husika.

(2) Shughuli za ukusanyaji, uzoaji, urejelezaji na utumiaji tena wa taka zinaweza kufanywa na Halmashauri au wakala wake kwa kadiri watakavyokubaliana.

Taka za hospitali

25. Ukusanyaji, uhifadhi na uteketezaji wa taka za hospitali na dawa zilizofikia ukomo wa matumizi utafanyika kutokana na taratibu zilizowekwa na Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya.

Udhibiti wa taka gesi

26. Halmashauri itadhibiti uzalishwaji wa taka gesi kwa-

(a) kutenga maeneo maalum ya ujenzi wa viwanda vinavyozalisha taka gesi eneo lililopo mbali na Makazi ya watu;

(b) kutoa elimu ya ujenzi wa nyumba za makazi zenye nafasi wazi za kutosheleza kuingiza na kutoa hewa na kupiga marufuku matumizi ya samadi ndani ya nyumba kama nishati ya kupikia.

Wachuuzi wa miwa, matunda na mboga mboga

27.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mchuuzi wa miwa, matunda au mbogamboga kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya bidhaa zake.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya biashara ya miwa, matunda au mbogamboga pembeni mwa barabara au katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Udhibiti wa Taka zinazozalishwa kutoka katika vyombo vya usafiri

28. (1) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma hawataruhusiwa kutupa taka nje ya vyombo wanavyotumia na taka zote zitawekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo husika.

(2) Mtu yeyote akiwa ndani ya gari au mabasi, au chombo chochote cha usafiri hataruhusiwa kutupa nje kitu chochote au taka.

Chukizo au kero

29.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuweka au kujenga au kutelekeza kitu chochote kinachoweza kusababisha kero au kilicho katika hali ya uchafu ambacho kinaweza kusababisha-

(a) madhara kwa maisha ya Binadamu, Wanyama au viumbe hai wengine;
(b) adha, kero, chukizo au kelele kwa watu wengine; au
(c) magonjwa.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuweka mtambo au mashine au gari, pikipiki au chombo chochote kinachoweza kuchafua hewa kwa kutoa moshi mzito au mwingi unaosababishwa na uchakavu wa chombo chenyewe.

Huduma ya maeneo ya kutupa taka

30.-(1) Halmashauri itatenga, itajenga na kuendesha vitu vya kukusanyia taka ngumu (collection points) maeneo ya kutunza taka kwa muda kabla ya kusafirisha kwenda dampo au dampo la kisasa au eneo la kurejelesha.

(2) Halmashauri inaweza kumpa wakala au kuingia ubia katika kujenga na kuendesha maeneo ya kuteketezea au kurejelesha taka ngumu.

(3) Wamiliki au wapangaji au wakazi wa maeneo ya makazi na biashara watalipia ada ya ukusanyaji na uzoaji taka ngumu kwa mujibu wa viwango

vitakavyowekwa na kutangazwa na Halmashauri.

Zuio la kufanya shughuli katika madampo

31.Mtu yeyote, taasisi au kikundi hakitaruhusiwa kufanya shughuli yoyote katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kukusanyia taka isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Halmashauri.

Uhifadhi maji taka

32.-(1)Kila mmiliki wa nyumba atahakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kufungulia na kutiririsha maji taka au kinyesi kutoka chooni au sehemu yoyote wakati wa mvua au wakati wowote kwenye mifereji ya maji ya mvua, mabonde au maji yanayotembea au sehemu nyingine yoyote isiyoruhusiwa.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

33.-(1) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji atahakikisha kwamba-

(a) nyumba yake ina choo safi, imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo; na
(b) anaweka sehemu maalum ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni maalum ya kimiminika.

(2) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini kutoka chanzo chochote cha maji.

Vyoo vya umma

34.-(1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa kiwe cha kudumu na-

(a) matundu yasiyopungua mawili kwa wanawake na mawili kwa wanaume;
(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa

maji ya kutosha yaliyo safi na salama;

(c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba;

(d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake;

(e) kuwepo na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na

(f) kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

35. Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu na atatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

36. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsi zote.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

37. Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika na kuchafua mazingira.

Mabaki ya ujenzi

38. Mtu yeyote hataruhusiwa kubomoa au kusababisha kubomoka kwa jengo au sehemu ya jengo bila kutoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri siku saba kabla ya kubomoa jengo.

Maegesho na matengenezo ya magari na mitambo

39.-(1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika katika karakana, gereji au maeneo maalum yaliyoruhusiwa na Halmashauri.

(2) Mtu yeyote hatoruhusiwa kuegesha gari bovu, au kufanya matengenezo, au kuosha gari, pikipiki, au mtambo wowote kwenye eneo la Barabara, hifadhi ya Barabara, njia ya waenda kwa miguu, mtaa, maeneo ya wazi, kando ya mito au maziwa, au eneo lolote ambalo halikutengwa kwa shughuli za aina hizo.

Udhibiti wa wadudu waharibifu na waenezao magonjwa

40.-(1) Kila mmiliki wa nyumba au jengo lolote atahakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji yaliyotuama, maji machafu, takataka, au kitu kingine chochote kinachoweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara ya afya binadamu.

(2) Mtu yeyote anayetaka kupulizia dawa ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba, jengo au mahali popote atalazimika kutoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri.

Usafi wa machinjio na maduka ya nyama

41.-(1) Halmashauri itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika machinjio na kuhakikisha kuwa machinjio zimetengenezwa kwa kiambaza cha saruji, mifugo inachinjwa katika machinjio hizo, upatikanaji wa huduma ya maji safi, na kutengwa maeneo maalumu ya kukusanyia taka.

(2) Wahudumu wa bucha za nyama na samaki watatakiwa kufanya biashara katika bucha zilizo katika hali ya usafi na watatakiwa kuvaa nguo safi nyeupe na kufunika vichwa kwa kofia.

Siku ya usafi wa mazingira

42.-(1) Halmashauri itatenga siku maalum itakayojulikana kuwa ni siku ya usafi wa mazingira ambapo watu wote watashiriki katika kufanya usafi wa maeneo ya umma na makazi.

(2) Siku hii inaweza kutumika kama siku maalum ya kutoa elimu ya usafi na mazingira kwa umma na kutoa tuzo kwa mtu yeyote, taasisi au Asasi

ambayo imeshiriki vyema katika usafi na utunzaji wa mazingira.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), kila mtu ataendelea kutekeleza wajibu wa kufanya usafi wa kila siku katika eneo lake.

Uwezo wa kukagua

43.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi na wakati wowote inapotakiwa kufanyika kwa ukaguzi maalumu kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii

44. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

45. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

Ilani ya kuondoa kero

46.-(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa

kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Uteuzi wa wakala

47.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala wa kukusanya ada kwa niaba yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hii -

(a) atakuwa na wajibu wa kukusanya, kwa niaba ya Halmashauri, ada mbalimbali zinazohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira, katika eneo lake alilopangiwa na kwa viwango vilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii;

(b) atakusanya ada kwa kutumia mfumo wa kielekitroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri; na

(c) Atatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya mkataba.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa

48. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo-

(a) atatupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.

(b) atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;

(c) atamwaga taka barabarani, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(d) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(e) ataacha nyumba anayoishi au kumiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo;

(f) ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;

(g) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(h) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni, upenuni;

(i) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri;

(j) ataingiza mfugo au mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(k) atasafirisha mfugo au mifugo bila kuwa na kibali;

(l) atalisha mfugo au mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(m) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo (kokoro);

(n) ataharibu chanzo cha maji au kushindwa

kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.

(o) atabainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe hai wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

(p) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;

(q) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti, iliyohifadhiwa kama bustani ya miti, msitu ya asili au iliyopandwa kwa ajili ya hifadhi;

(r) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;

(s) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali; au

(t) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Adhabu

49. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.

kufilililisha kosa

50. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza

fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 20(1))*

ADA YA KUZOA TAKA

| Namba. | Aina ya biashara | Viwango vya Ada |
|---|---|---|
| 1. | Makazi (Kaya) | 5,000/= kwa mwezi |
| 2. | Mgahawa mkubwa | 10,000/= kwa mwezi |
| 3. | Zahanati (taka zisizo hatari) | 10,000/= kwa mwezi |
| 4. | Kituo cha afya (taka zisizo hatari) | 15,000/ kwa mwezi |
| 5. | Hospitali | 30,000/= kwa mwezi |
| 6. | Hospitali ya rufaa | 70,000/= Kwa mwezi |
| 7. | Kiwanda cha kuuza mbao | 20,000/= kwa mwezi |
| 8. | Fundi seremala | 5,000/= kwa mwezi |
| 9. | Fundi chuma | 5,000/= kwa mwezi |
| 10. | Karakana | 20,000/= kwa mwezi |
| 11. | Kiwanda kidogo | 20,000/= kwa mwezi |
| 12. | Kiwanda kikubwa | 200,000/= kwa mwezi |
| 13. | Duka la jumla | 20,000/= kwa mwezi |
| 14. | Duka la rejereja/huduma | 5,000/= kwa mwezi |
| 15. | Shule ya Msingi ya Bweni (binafsi) | 20,000/= kwa mwezi |
| 16. | Shule ya msingi ya kutwa (binafsi) | 10,000/= kwa mwezi |
| 17. | Shule ya Sekondari ya kutwa (binafsi) | 15,000/= kwa mwezi |
| 18. | Shule ya Sekondari ya Bweni (binafsi) | 30,000/= kwa mwezi |
| 19. | Kituo cha kulelea watoto | 5,000/= kwa mwezi |
| 20. | Kituo cha kutunzia watu wenye mahitaji maalum | 5,000/= kwa mwezi |
| 21. | Duka dogo la chakula | 5,000/= kwa mwezi |
| 22. | Duka kubwa la chakula | 10,000/= kwa mwezi |
| 23. | Baa | 10,000/= kwa mwezi |
| 24. | Klabu ya usiku | 20,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 25. | Kumbi za Sherehe | 30,000/= kwa mwezi |
| 26. | Duka la kuuza nyama na samaki | 10,000/= kwa mwezi |
| 27. | Duka la dawa (Jumla na Rejareja) | 20,000/= kwa mwezi |
| 28. | Duka la dawa (Rejareja) | 10,000/= kwa mwezi |
| 29. | Kiwanda kidogo kwa trip zisizozidi 4 kwa mwezi | 50,000/= Kwa mwezi |
| 30. | Dobi mdogo | 2,000/= kwa mwezi |
| 31. | Dobi mkubwa | 10,000/= kwa mwezi |
| 32. | Fundi wa vifaa vya umeme | 5,000/= kwa mwezi |
| 33. | Fundi kushona kwa kila cherehani | 3,000/= kwa mwezi |
| 34. | Saluni | 10,000/= kwa mwezi |
| 35. | Kituo cha kuuza mafuta | 30,000/= kwa mwezi |
| 36. | Stoo | 5,000/= kwa mwezi |
| 37. | Ghala | 30,000/= kwa mwezi |
| 38. | Hoteli: | |
| | (a) ya kitalii | 100,000/= kwa mwezi |
| | (b) ya kawaida | 50,000/= kwa mwezi |
| | (c) nyumba ya kulala wageni (Guest house) | 20,000/= kwa mwezi |
| 39. | Taasisi | 100,000/= kwa mwezi |
| 40. | kilabu ya pombe ya asili | 2,000/= kwa mwezi |
| 41. | Dahalia | 10,000/= kwa mwezi |
| 42. | Kituo cha michezo | 5,000/= kwa mwezi |
| 43. | Uwanja wa michezo | 20,000/= kwa mwezi |
| 44. | Washona viatu:<br>Katikati ya mji<br>Pembezoni mwa mji | <br>2,000/= kwa mwezi<br>1,000/= kwa mwezi |
| 45. | Stoo za mkaa | 10,000/= kwa mwezi |
| 46. | Mama lishe/Baba lishe | 5,000/= kwa mwezi |
| 47. | Duka la kuuza Magari | 20,000/= kwa Mwezi |
| 48. | Vituo vya kuoshea magari | 10,000/= kwa mwezi |
| 49. | Mashamba makubwa ya maua, kahawa na mazao mengine. | 100,000/= kwa mwezi |
| 50. | Kupima afya Wahudumu wa Migahawa, Hotel, Nyumba za kulala wageni, shule, Baa na Vilabu vya pombe; | 3,000/= kwa kila muhudumu kila baada ya miezi mitatu |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 45)(2))*

ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa aya ya 45 cha Sheria Ndogo ya Usafi na Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji, ya Mwaka 2024.

SEHEMU 'A'

Ndugu…………………........wa Mtaa/Kijiji…………Kata ya…………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi………..mwaka….Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma ya …………………….. iliyopo katika eneo la ………………katika Kitongoji/Mtaa*………. Kijiji cha……………Kata ya………….

Imekutwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(1) ……………………………………………………………………………

(2) ……………………………………………………………………………

SEHEMU 'B'

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu 'A' ya Ilani hii,

SEHEMU 'C'

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe………………. endapo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

...................................................

JINA:

Afisa Muidhiniwa.

| IMETOLEWA NA:- | IMEPOKELEWA NA:- |
|---|---|
| Jina: ............................ | Jina: ............................. |
| Sahihi: ....................... | Sahihi: .......................... |
| Wadhifa: ................... | Wadhifa: ....................... |
| Tarehe:...................... | Tarehe: ......................... |

## JEDWALI LA TATU

*Limetengenezwa chini ya aya ya 46(1)*

### ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za (Afya, usafi na Hifadhi ya mazingira ) za Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji ,2024.

SEHEMU "A"

Ndugu .................................................... wa S.L.P .................................unaarifiwa kwamba katika ukaguzi wa ...................................................... uliofanyika tarehe..............mwezi wa ...........................mwaka ......................... katika nyumba yako ya .................................. Biashara/kuishi/kutolea huduma/ kiwanja iliyopo eneo la ......................................... kumekutwa machukizo/kero/Uchafu kama ifuatavyo:-

1)...............................................................

2) ..............................................................

3) ...............................................................

SEHEMU "B"

Kwa ilani hii unaamuriwa kurekebisha /kuondoa/kusafisha kwa:-

1)...............................................................

2) ..............................................................

3) ...............................................................

SEHEMU "C"

Unapewa muda wa siku .......... tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu "B" ya ilani hii , kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimikakukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

...................................................

JINA:

Afisa Muidhiniwa.

| IMETOLEWA NA:- | IMEPOKELEWA NA:- |
| --- | --- |
| Jina: ............................ | Jina: ............................. |
| Sahihi: ....................... | Sahihi: .......................... |
| Wadhifa: ................... | Wadhifa: ....................... |
| Tarehe:...................... | Tarehe: ......................... |

JEDWALI LA NNE

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 50)*

KUFILILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwamba mnamo tarehe……………ya mwezi……………..Mwaka ……………………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya ………………………cha Sheria Ndogo ya (Usafi na Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji ya Mwaka 2024.
Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji. niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe…ya Mwezi……………Mwaka…….
Jina…………………………………..…..
Saini……………………………….…..….

Mbele ya:
Jina………………………………………….
wadhifa………………………………………
Saini……..…………………………………..
Tarehe: ……………………………………..

Dodoma,
……………., 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa*

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma ujiji imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujiji kilichofanyika Tarehe 04 mwezi 10 Mwaka 2022

MWANTUM H. MGONJA
*Mkurugenzi*

*Halmashauri ya Mji Mafinga*

REGNANT Z. KIVINGE
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Mji Mafinga*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*